# Standard 4 End Term 1 Exam, 2016

## KISWAHILI

**MUDA: SAA 1 DAK. 40**

**Soma kifungu kifuatacho kisha uchague jibu lifaalo kujazia pengo zilizoachwa**

Siku ____1____ mzee Sokota ____2____ akimpeleka mbuzi ____3____ sokoni. ____4____ njiani alikutana na kijana ____5____ aliyemuuliza kwa mshangao "Mzee! Unampeleka Simba wapi ____6____ " Mzee alipuuza maneno haya na kusema, "Huo ni ____7____ huyu ni mbuzi".

Mzee alitembea hatua ____8____ tu akakutana na kijana mwingine ____9____ na kusema. "Ewe mzee ____10____ Fisi, unampeleka wapi? "Mzee Sokota aliposikia hivyo alishtuka sana na kuanza ____11____ mbuzi chini alijawa na ____12____ na ____13____ . kushindwa kama ____14____ mbuzi alikuwa Simba, Fisi ____15____ Mbuzi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kimoja | B. mmoja | C. moja | D. monja |
| 2. | A. alikuwa | B. alikua | C. alikuwako | D. alikuwanga |
| 3. | A. yake | B. wake | C. lake | D. zake |
| 4. | A. Akiona | B. Akitembeanga | C. Akiwanga | D. Akiwa |
| 5. | A. mojamoja | B. monja | C. moja | D. mmoja |
| 6. | A. ? | B. ! | C. , | D. : |
| 7. | A. upusi | B. upuuzi | C. ubuzi | D. umbusi |
| 8. | A. kidogo | B. kidogo kidogo | C. cheche | D. mbali |
| 9. | A. aliyeshongea | B. aliyekaarika | C. aliyefurahi | D. aliyekimbia |
| 10. | A. humo ogopangi | B. humwogopi | C. huogopangagi | D. hupoteangi |
| 11. | A. kumfikiria | B. kumwangalia | C. kumchunguza | D. kumuuza |
| 12. | A. bashasha | B. furaha | C. wasiwasi | D. kushindwa |
| 13. | A. akaanza | B. akaamua | C. akaona | D. akafiri |
| 14. | A. uongo | B. ndio | C. ndiye | D. kweli |
| 15. | A. tena | B. au | C. si | D. pengine |

**Kutoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo**

16 Watu huagana vipi usiku?
A. Tuonane B. Alamsiki
C. Habari D. Ndoto mbaya

17. Jina 'kiroboto' liko katika ngeli ipi?
A. A - WA B. KI - VI
C. I - ZI D. LI - YA


18. **Kamilisha sentensi ifuatayo**
Ningekusaidia ________ sina uwezo.
A. wala B. kwa sababu C. lakini D. na

19. Samaki huishi majini kama vile ng'ombe huishi katika ____________
A. kizimba B. kombe
C. zizi D. mzinga

20. Sehemu ya mwili inayosaidia kupumua huitwa?
A. nyongo B. ini
C. moyo D. pua

21. **Kamilisha methali ifuatayo**
Mchimba kisima ________
A. hunywa maji B. huingia mwenyewe
C. ana uma D. huchoka sana

22. Upande uliochorwa X huitwa __________





A. magharibi
B. kaskasini
C. kusini
D. mashariki

23. Ni neno gani halifai miongoni mwa mengine?
A. Heroe B. mbayuwayu
C. kipanga D. kulungu

24. $^{1}/_{6}$ huitwa ____________
A. subui B. sudusi
C. tusui D. humusi

25. Utamwitaje mtoto wa dada yako?
A. Shemeji B. Wifi
C. Mpwa D. Binamu

26. Maumbo haya huitwa____________



A. mstatili, pia
B. mraba, pia
C. mraba, duara
D. molo, pia

Kiswahili Exam compiled by Schools Net Kenya, End Term 1, 2016
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227

27. Ugonjwa unaosababishwa na konokono wa majini huitwa ______________
A. kichocho B. kifaduro
C. kifafa D. ukimwi

28. _______ ni gari la baba.
A. Hii B. Hili C. Hizi D. Hiyo

29. Wakati wa kiangazi mimea ______ maji isikauke.
A. humwagiliwa B. hunyunyiziwa
C. huokokewa D. hutolewa

30. **Andika katika wingi**
Yeye hutumia kisu kikali
A. Nyinyi hutumia visu vikali
B. Wewe hutumia visu vikali
C. Wao hutumia visu vikali
D. Sisi hutumia visu vikali

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31-40**

Sungura alikuwa amewadanganya wanyama wenzake kwa siku nyingi. Alitumia ujanja wake kuwafanya wenzake wajinga. Alisababisha wengi wapigwe na hata kuuawa. Waliamua kumkomesha sungura na ujanja wake.

Wanyama walipatana na kutoa malalamishi yao. Aliyeteseka ni Fisi aliyedanganywa kwamba mkono wa binadamu ungeanguka. Alimfuata binadamu bila kujua alingojewa na kipigo cha kumvunja mbavu. Wanyama wote walimsikitikia Fisi sana. Fisi tena aliraruliwa ngozi na simba mgongoni ati atoe kitambaa cha kufunga **jeraha**. Aidha Sungura alikataa kuchimba kisima cha maji na akaendelea kuiba maji msimu wa ukame. Wote kwa pamoja waliona ni heri afe. Chui ndiye alikuwa kiongozi wa mkutano naye mzee Kobe akitoa ushauri.

31. Sungura alikuwa amewadanganya wenzake
A. siku chache B. kidogo
C. siku nyingi D. hatujui

32. Sungura alitumia nini kuwafanya wanyama wengine kuwa wajinga?
A. Ujanja B. Masomo
C. Akili D. Simu

33. Kwa pamoja wanyama wote waliamua?
A. Kumwadhibu sungura B. Kumuua
C. Kumsamehe D. Kumkomesha

34. Wanyama walipokutana______________
A. walikasirika sana
B. walikuwa na furaha
C. walitoa malalamishi yao
D. walitoa mtego

35. Wanyama walioteswa kwa ujanja wa Sungura ni
A. Fisi B. Wengi C. Kobe D. Chui

36. Fisi aliteswa mara ngapi?
A. Moja B. Mbili C. Sita D. Tatu

37. Fisi aliraruliwa ngozi mgongoni na Simba
A. Akidhani kwamba ni kitambaa
B. Kwa sababu alikataa kutoa kitambaa cha kufunga jeraha
C. Kwa sababu ilipendeza
D. Kwa kuwa aliumia

38. Neno jeraha linamaanisha
A. kidonda B. maumivu C. huvunjika D. jicho

39. Wanyama waliposikia mateso ya Fisi
A. walifurahi sana B. walishangilia
C. walifedheheka D. walihuzunika

40. Mkutano wa wanyama ulifanyika wapi?
A. Msituni B. Kwa chui
C. Kwa mzee Kobe D. Hatujui

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41-50**

Katika kijiji cha Waso paliishi mzee mmoja aliyeitwa Mtoro. Mzee huyu alikuwa mwenye tabia nzuri, tena mple sana. Alipendwa na majirani zake wote nao walikuwa wakimwendea ili wapate mawaidha juu ya mambo na hasa wakiwa na matatizo ya kinyumbani.

Mzee Mtoro alikuwa na mke mmoja aliyekuwa amezaa naye mtoto mmoja tu. Mtoto huyo alikuwa ni msichana na aliitwa Mrembo. Mrembo alikuwa vile jina lilivyo. Yaani mzuri kwelikweli, sura nzuri, umbo na tabia. Pia watu wa kijiji chake walimpenda kama vile walivyompenda baba yake.

Familia hii ilikuwa ikiishi maisha ya raha, furaha na amani. Kwa bahati mbaya, siku moja mama yake Mrembo alichikwa na maradhi ya kipindupindu na baada ya kuugua kwa siku chache alifariki dunia. Jambo hili lilimhusunisha sana baba yake Mrembo na wanakijiji wote kwa jumla.

41. Kijiji hiki kiliitwa
A. Sowa B. Waso C. Mtoro D. Mrembo

42. Mzee aliitwa ______________
A. Mtemi B. Mtoro C. Waso D. Mrembo

43. Majirani walimwendea Mtoro ili
A. wabarikiwe B. wamfurahishe
C. wapewe mawaidha D. awapende

44. Mzee huyu alikuwa na wake wangapi?
A. Mmoja B. Wawili
C. Hakuwa ameoa D. Watatu

45. Mtoto wa Mtoro alikuwa _____________
A. mjeuri B. mrembo
C. mbaya D. mchokozi

46. Bahati mbaya iliyoipata familia hii ni
A. Mrembo kufa
B. Mtoro kufa
C. Wote kufa
D. Mamaye Mrembo kufa

47. Mamaye Mrembo aliugua ugonjwa gani?
A. Malaria B. Ukimwi
C. Kipindupindu D. Kifuakikuu

48. Mrembo alikuwa na tabia
A. mbaya B. za utundu
C. nzuri D. za washerati

49. Baba yake Mrembo alihuzunishwa sana na nini?
A. Kifo cha mkewe
B. Kuzaliwa kwa Mrembo
C. Wanakijiji kumpenda
D. Kutukanwa na mkewe

50. Kichwa kifaacho taarifa hii ni_____
A. Mtoro na familia yake
B. Mtoto kuzaliwa
C. Bibiye Mtoro kufa
D. Kifo cha Mrembo